

**MATATIZO YA LEKSIKOGRAFIA -
TAFSIRI: TATHMINI YA KAMUSI
YA F. JOHNSON (1939) //**

PATRICK IRIBE MWANGI

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA
BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA M. A.
KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

1996

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY



0146642 4

MUHTASARI

Tasnifu yetu imejengwa katika msingi unaoafiki kuwa kamusi za lugha mbili ni kazi halisi za tafsiri. Tahakiki nyingi ambazo tayari zimeandikwa kuhusu matatizo ya tafsiri zimeegemea zaidi katika fasihi na kazi za kidini. Sisi tunaonyesha kuwa hata kamusi za lugha mbili zina matatizo mengi ya tafsiri katika ngazi mbalimbali za lugha. Tasnifu yenyewe imegawanywa katika sura tano.

Katika sura ya kwanza, tumelifafanua somo letu la utafiti ambalo ni leksikografia-tafsiri. Pia, tumeonyesha madhumuni yetu katika utafiti huu na sababu zilizotufanya tuchague somo hili. Fauka ya haya, tumeelezea upeo na mipaka ya tasnifu yetu na pia yale yaliyoandikwa kuhusu somo hili. Tumefafanua pia mwongozo wa utafiti wetu na nadharia tete. Mwisho, tumeeleza njia tutakazozitumia katika utafiti wetu.

Katika sura ya pili, tumeifafanua dhana ya tafsiri huku tukionyesha matatizo, umuhimu na nafasi yake. Aidha, tumeifafanua dhana ya leksikografia ambapo tumeeleza maana ya kamusi, mambo muhimu katika kamusi na aina za kamusi. Hatimaye tumeifafanua dhana ya leksikografia-

tafsiri huku tukionyesha wale ambao hunufaisha na kamusi za lugha mbili. Mwisho, tumeonyesha nafasi ya maana katika tafsiri ya moja kwa moja, tafsiri-huru na tafsiri-mawasiliano.

Sura ya tatu inahusu mambo ya sarufi katika kamusi za uwili lugha. Tumeonyesha aina za sarufi, kisha tumefafanua kuhusu matatizo ya kifonolojia katika kamusi za uwili lugha na pia yale ya kimofolojia na kisintaksi. Hatimaye, tumetoa mifano ya tafsiri zisizo sahihi kimofolojia na kisintaksi katika kamusi ya Johnson (1939) ya Kingereza-Kiswahili ambayo tunaitathmini.

Sura ya nne ndiyo kiini cha kazi yetu. Tumeijadili dhana ya semantiki, maana katika semantiki na pia matatizo ya kisemantiki katika kamusi za uwili lugha. Matatizo haya yanahusu uchaguzi wa visawe, uchanganuzi wa maana, maneno ya jamii moja na ufafanuzi wa kimichoro na kimifano. Hatimaye tumeyaonyesha matatizo hayo kama yalivyojitokeza katika kamusi ya F. Johnson (1939). Tumeonyesha pia makosa ya kisemantiki katika mifano iliyotolewa na mtunzi na matatizo mengine ya jumla katika kamusi hiyo.

(xii)

Sura ya tano ni hitimisho. Tumeonyesha kwa kifupi yale tuliyoyashughulikia, yaliyojitokeza kuhusu nadharia-tete, ufaaji wa mwongozo wetu wa utafiti, matatizo tuliyoyapata na kisha tunatoa mapendekezo yetu.